# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 2328

Jina la Chapisho: Muhtasari wa Elimu ya Dini ya Kiislamu Elimu ya Msingi Darasa la III-VI

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Jumuiya ya Ufundishaji wa Masomo ya Kiislamu Tanzania

ISBN: 978-9912-9958-6-4

Muhtasari huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 4 Mei 2026 kuwa Muhtasari wa Elimu ya Dini ya Kiislamu Elimu ya Msingi Darasa la III-VI nchini Tanzania.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

# MUHTASARI WA ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

# ELIMU YA MSINGI DARASA LA III-VI

2026

© Jumuiya ya Ufundishaji  wa Masomo ya Kiislamu Tanzania, 2026

Toleo la Kwanza, 2026

ISBN: 978 - 9912 - 9958 - 6 - 4

Jumuiya ya Ufundishaji wa Masomo ya Kiislamu Tanzania (TISTA)
S.L.P 55104,
Dar es Salaam, Tanzania
Simu:  +255 784 267 762
Barua pepe:  islamicstudies@tista.or.tz
Tovuti:  www.tista.or.tz

Umechapishwa na:
Taasisi ya Elimu Tanzania

Muhtasari huu urejelewe kama: Jumuiya ya Ufundishaji wa Masomo ya Kiislamu Tanzania (2026*), Muhtasari wa Elimu ya Dini ya Kiislamu Elimu ya Msingi  Darasa la III-VI.* Jumuiya ya Ufundishaji wa Masomo ya Kiislamu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha wala kutafsiri andiko hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Jumuiya ya Ufundishaji  wa Masomo ya Kiislamu Tanzania (TISTA)

# Yaliyomo


Orodha ya majedwali . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . iv

Vifupisho . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . v

Shukrani . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . vi

1.0 Utangulizi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1

2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1

3.0 Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la III-VI. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1

4.0 Umahiri wa jumla wa Elimu ya Msingi Darasa la III-VI . . . . . . . . . . . . . 2

5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 3

6.0 Mzazi/Mlezi katika Ufundishaji na Ujifunzaji.. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 3

6.1 Mwalimu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 3

6.2 Mwanafunzi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 4

6.3 Mzazi/mlezi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 5

6.4 Jamii . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 5

7.0 Mbinu za Ujifunzaji na Ufundishaji Zinazopendekezwa . . . . . . . . . . . . . . 5

8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji Zinazopendekezwa . . . . . . . . . . . . . . . 5

9.0 Upimaji . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 6

10.0 Idadi ya Vipindi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 6

11.0 Maudhui ya ufundishaji na ujifunzaji. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 6

Darasa la III . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 7

Darasa la IV . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 12

Darasa la V . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 18

Darasa la VI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 23

Bibliografia .. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 28

## Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 1 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi kwa Darasa la III-VI . . . . . . . . . 3

Jedwali Na.2 Maudhui ya Darasa la III . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 7

Jedwali Na.3 Maudhui ya Darasa la 1V . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 11

Jedwali Na.4 Maudhui ya Darasa la V . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 17

Jedwali Na.5 Maudhui ya Darasa la VI. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 22

**Vifupisho**

| | |
|---|---|
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| TISTA | Tanzania Islamic Studies Teaching Association |

## Shukurani

Kila sifa njema anastahiki Allah (*subhaanahu Wata'ala*) Mola Mlezi wa viumbe vyote. Rehema na amani zimuendee Mtume wetu Muhammad (*Swallallaahu 'Alayhi Wasallam*), Maswahaba zake pamoja na wafuasi wake wote.

Maandalizi ya Muhtasari wa Elimu ya Dini ya Kiislamu ngazi ya Elimu ya Msingi Darasa la III-VI yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za Kiislamu. Jumuiya ya Ufundishaji wa Masomo ya Kiislamu Tanzania (TISTA) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha kupatikana kwa muhtasari huu. Wataalamu hawa wamefanya kazi kwa weledi mkubwa kuhakikisha kuwa maudhui ya muhtasari huu yanalenga kuwaandaa wahitimu wenye maarifa, ujuzi, maadili mema na stadi zitakazowawezesha kuishi maisha yenye maadili mema na kumudu maisha yao ya kila siku, ambalo ndilo lengo kuu la Uboreshaji wa Mitaala ya Mwaka 2023.

Mwisho, TISTA inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania kwa kuwezesha uandaaji na usambazaji wa muhtasari huu.



Sheikh, Dkt.Abubakar Zubeir Bin Ally Mbwana

Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania

**Kiongozi Mkuu**

**Jumuiya ya Ufundishaji wa Masomo ya Kiislamu Tanzania**

**1.0 Utangulizi**

Elimu ya Dini ya Kiislamu ni somo la lazima kwa wanafunzi waislamu wa ngazi ya Elimu ya Awali na Msingi Darasa III-VI nchini. Lengo la kufundisha somo hili ni kumjenga mtoto awe mcha Mungu na muadilifu katika maisha yake. Muhtasari huu umeandaliwa kwa lengo la kumwongoza mwalimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa Elimu ya Dini ya Kiislamu ngazi ya Elimu ya Msingi Darasa la III–VI, Tanzania Bara. Aidha, muhtasari utamwezesha mwalimu kupanga shughuli za ufundishaji na ujifunzaji kwa kumjengea mwanafunzi stadi za udadisi, ubunifu, ushirikiano, mawasiliano na utatuzi wa changamoto. Muhtasari huu umetafsiri Mtaala wa Elimu ya Msingi wa Mwaka 2023 ambao msingi wake mkuu umejikita kupata wahitimu wenye maarifa, ujuzi na stadi zitakazowawezesha kumudu maisha yao ya kila siku.

## 2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania

Malengo makuu ya Elimu Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;

(b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;

(c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;

(d) Kuelewa na kulinda tunu za taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya taifa;

(e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;

(f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;

(g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na

(h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

**3.0 Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la III – VI**

Malengo ya Elimu ya msingi Darasa III - VI ni kumwezesha mwanafunzi:

(a) Kukuza stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu na kuwasiliana kwa lugha fasaha, Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) na mawasiliano mguso;

(b) Kuifahamu, kuitumia na kuithamini lugha ya Kiswahili, Kiingereza, na angalau lugha nyingine moja ya kigeni;

(c) Kuthamini na kudumisha utamaduni wa Mtanzania, umoja wa kitaifa na kutambua tamaduni nyingine;

(d) Kukuza maarifa, uwezo wa kudadisi, kufikiri kiyakinifu, kubuni na kutatua matatizo;

(e) Kukuza maadili, uadilifu, na kuheshimu tofauti za imani;

(f) Kubaini na kukuza vipaji, vipawa, stadi za kazi, michezo na sanaa;

(g) Kukuza tabia ya kuthamini na kupenda kufanya kazi;

(h) Kutambua na kutumia sayansi na teknolojia katika kujifunza na maisha ya kila siku;

(i) Kukuza maarifa, ujuzi na mwelekeo wa kutunza mazingira, kuheshimu usawa wa kijinsia na masuala mengine mtambuka; na

(j) Kukuza uwezo wa kuchangamana katika mazingira jumuishi.

**4.0 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Msingi Darasa la III - VI**

Umahiri wa jumla utakaojengwa na mwanafunzi wa Darasa la III - VI ni:

(a) Kutumia stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu na kuwasiliana kwa lugha fasaha, Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) na mawasiliano mguso;

(b) Kutumia na kuithamini lugha ya Kiswahili, Kiingereza, na angalau lugha nyingine moja ya kigeni;

(c) Kuonesha, kuthamini na kuheshimu utamaduni wa Mtanzania, umoja wa kitaifa na kutambua tamaduni nyingine;

(d) Kudadisi, kufikiri kiyakinifu, kubuni na kutatua matatizo;

(e) Kuonesha uadilifu na kuheshimu tofauti za imani;

(f) Kutumia vipaji, vipawa, stadi za kazi, michezo na sanaa katika miktadha mbalimbali;

(g) Kuthamini na kupenda kufanya kazi;

(h) Kutumia sayansi na teknolojia katika kujifunza na maisha ya kila siku;

(i) Kutunza mazingira, kuheshimu usawa wa kijinsia na masuala mengine mtambuka; na

(j) Kuchangamana katika mazingira jumuishi.

## 5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi

Umahiri mkuu na umahiri mahususi unaotarajiwa kujengwa kwa Darasa la III-VI umebainishwa katika Jedwali Na. 1

**Jedwali Na.1 :** *Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Darasa la III-VI*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|
| 1.0 Kuishi kwa kumpwekesha Allah (*Suhaanahu Wata'ala*) | 1.1 Kufafanua nguzo za imani |
| | 1.2 Kuchambua dhana ya shirki |
| 2.0 Kuthamini Qur'an na mafundisho yake | 2.1 Kumudu misingi ya kufahamu na kusoma Qur'an |
| | 2.2 Kusoma na kutafsiri sura teule |
| 3.0 Kutekeleza ibada | 3.1 Kufafanua utekelezaji wa ibada ya swala |
| | 3.2 Kufafanua utekelezaji wa ibada ya swaumu |
| | 3.3 Kuishi kwa kumuiga Mtume Muhammad (*Swallallaahu'Alayhi Wasallam)* |
| 4.0 Kuthamini na kutumia Historia ya Uislamu | 4.1 Kutambua mitume wa Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) waliotajwa katika Qur'an |
| | 4.2 Kufafanua namna Mtume Muhammad (*Swallallaahu'Alayhi Wasallam*) alivyofundisha Uislamu |

## 6.0 Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi , Mzazi/Mlezi na Jamii katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji unategemea ushirikiano madhubuti baina ya mwalimu, mwanafunzi, mzazi/mlezi na jamii katika kutekeleza majukumu mbalimbali. Majukumu yao ni kama yafuatayo:

### 6.1 Mwalimu

Mwalimu anatarajiwa:

(a) Kumwezesha mwanafunzi kujifunza na kupata umahiri uliokusudiwa katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu;

(b) Kutumia mbinu za kufundishia na kujifunzia kwa kuzingatia umri, mahitaji anuai na uwezo wa mwanafunzi ili kumwezesha:

(i) kujenga umahiri unaohitajika katika karne ya 21; na

(ii) kushiriki kikamilifu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji

(c) Kutumia mbinu shirikishi zinazomfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji zikiwemo zile zinazomwezesha mwanafunzi kufikiri, kutafakari na kutafuta maarifa katika vyanzo mbalimbali. Mbinu za kufundishia na kujifunzia zinazopendekezwa ni pamoja na kazi vitendo, utafiti, majaribio ya kisayansi, majadiliano na kazi mradi ziwe zinalenga kutatua matatizo halisi katika mazingira ya mwanafunzi. Aidha, mwalimu anahimizwa kutumia njia nyingine mbadala kulingana na muktadha uliopo ili kufanikisha ujenzi wa umahiri uliokusudiwa;

(d) Kuandaa darasa salama lenye mazingira rafiki ya kufundishia na kujifunzia;

(e) Kutengeneza na kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia;

(f) Kufanya upimaji endelevu mara kwa mara kwa kutumia zana na mbinu za upimaji na tathmini zinazopima nadharia na vitendo zikwemo bunguabongo, orodha hakiki, majaribio, dodoso, maswali ya ana kwa ana, mazoezi, kazi kwa vitendo (kazi binafsi na kazi za vikundi), kazimradi, na mkoba wa kazi, zana na mbinu nyingine ni majaribio kwa vitendo, mitihani ya muhula na mtihani wa mwisho;

(g) Kuhakikisha kuwa ufundishaji na ujifunzaji unafanyika kwa haki na usawa kwa kila mwanafunzi bila kujali tofauti zao;

(h) Kumlinda mwanafunzi awapo shuleni;

(i) Kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi ya kila siku;

(j) Kubaini mahitaji ya mwanafunzi na kutoa afua stahiki;

(k) Kushirikisha wazazi/walezi na jamii katika hatua mbalimbali za ujifunzaji wa mwanafunzi; na

(l) Kuchopeka masuala mtambuka na TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji.

### 6.2 Mwanafunzi

Mwanafunzi anatarajiwa:

(a) Kuwa mtendaji mkuu katika mchakato wote wa ujifunzaji;

(b) Kushiriki katika shughuli mbalimbali za ujifunzaji ndani na nje ya darasa ili kupata umahiri unaokusudiwa; na

(c) Kushiriki katika kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwemo vitabu vya kiada, ziada na machapisho mengine kutoka katika maktaba mtandao.

## 6.3 Mzazi/Mlezi

Mzazi /Mlezi anatarajiwa:

(a) Kusimamia na kufuatilia maendeleo ya mtoto katika ujifunzaji;

(b) Kumsimamia mtoto kutekeleza kazi zake za kitaaluma pale inapowezekana;

(c) Kuhakikisha kuwa mazingira ya nyumbani ni rafiki na salama yanayowezesha ujifunzaji;

(d) Kufuatilia mwenendo wa tabia ya mtoto;

(e) Kumpatia mwanafunzi vifaa vyote vinavyohitajika katika ujifunzaji;

(f) Kuhakikisha mwanafunzi anapata mahitaji muhimu; na

(g) Kumfundisha mtoto umuhimu na thamani ya elimu na kazi pamoja na kumuhimiza kujifunza kwa bidii.

## 6.4 Jamii

Jamii inatarajiwa:

(a) Kushirikiana na walimu katika kumlea mtoto

(b) Kutoa fursa kwa mtoto kujifunza mambo yenye manufaa

(c) Kuandaa mazingira wezeshi kwa mtoto kujifunza tunu za jamii zilizohifadhi utambulisho na utu wake.

## 7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji Zinazopendekezwa

Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji ni msingi katika kujenga umahiri wa mwanafunzi. Muhtasari huu unapendekeza mbinu za ufundishaji na ujifunzaji kwa kila shughuli. Miongoni mwa mbinu hizo ni ziara za kimasomo, kazimradi na kazi za vitendo. Hata hivyo, mwalimu anashauriwa kutumia mbinu nyingine kama hizo kulingana na muktadha wa ufundishaji na ujifunzaji.

## 8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji Zinazopendekezwa

Mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unahitaji zana/vifaa mbalimbali ili kujenga umahiri uliokusudiwa. Hivyo, mwalimu na mwanafunzi wanapaswa kushirikiana katika kuandaa na kufaragua zana/vifaa mbadala vinavyopatikana katika mazingira ya shuleni na nyumbani pindi vinapohitajika. Mwalimu na mwanafunzi wanapaswa kutafuta taarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali ili kuleta ufanisi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Mwalimu anapaswa kuhakikisha kuwa mwanafunzi anapata nafasi ya kuona, kunusa, kuonja, kusikia na kushika zana bila kuhatarisha afya na hali ya mwanafunzi.

## 9.0 Upimaji

Upimaji ni suala muhimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji ili kuwezesha ujenzi wa umahiri unaokusudiwa. Upimaji wa Elimu ya Dini ya Kiislamu utajumuisha upimaji endelevu na upimaji tamati. Upimaji endelevu utazingatia vigezo vya upimaji vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji na utamwezesha mwalimu kubaini uwezo na uhitaji wa mwanafunzi katika ujifunzaji. Vilevile, utalenga kupima mabadiliko katika maarifa, stadi na mwelekeo wa kutenda, kuthamini, na kutumia stadi anazojifunza katika mazingira yanayomzunguka. Aidha, mwalimu atatumia taarifa za upimaji kuboresha ufundishaji na kuwezesha wanafunzi kufikia lengo la ujifunzaji. Zana za upimaji zinazoweza kutumika wakati wa ufundishaji na ujifunzaji ni bunguabongo, orodha hakiki, mazoezi ya darasani, majaribio, majaribio kwa vitendo, dodoso, maswali ya ana kwa ana, mazoezi, kazi kwa vitendo (kazi binafsi na kazi za vikundi) kazimradi na mkoba wa kazi na zana nyingine kama hizo.

Upimaji tamati utahusisha mitihani ya wiki, mwezi, muhula na mtihani wa mwisho wa mwaka ambayo itatumika kupima maendeleo ya ujifunzaji wa mwanafunzi. Taarifa za upimaji huu pamoja na kutumika kutathmini maendeleo ya mwanafunzi, zitatumika kutoa mrejesho wa kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, kutakuwa na upimaji wa Kitaifa wa darasa la sita ambao utachangia alama 7.5% katika mtihani wa kidato cha Nne.

## 10.0 Idadi ya Vipindi

Muhtasari wa Elimu ya Dini ya Kiislamu ngazi ya Elimu ya Msingi Darasa la III-VI unatoa makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za kutendwa na mwanafunzi. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 40. Idadi ya vipindi kwa somo hili ni viwili (2) kwa wiki kwa Darasa la III-VI.

## 11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Maudhui ya ufundishaji na ujifunzaji yamepangiliwa katika jedwali lenye vipengele saba, ambavyo ni umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za ujifunzaji, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa, vigezo vya upimaji, zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa pamoja na idadi ya vipindi. Maudhui hayo yameoneshwa katika jedwali Na.2-5

## Darasa la III

**Jedwali Na. 2** *Maudhui ya Darasa la III*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughul za Ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kuishi kwa kumpwekesha Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) | 1.1. Kufafanua nguzo za imani | (a) Kubainisha nguzo za Imani kwa mpangilio wake | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi kisha waulize maswali kuhusu nguzo za imani | Kubainisha nguzo za Imani kwa mpangilio wake kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tatu | 8 |
| | | (b) Kusoma majina ya Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) 41-50 | **Onesho mbinu**: Tamka majina ya Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) 41-50 kwa sauti kwa kasi mwafaka kulingana na umri wa wanafunzi wako, (**matamshi sahihi**). Kisha waongoze wanafunzi kutamka | Kusoma majina ya Allah (*Subhaanahu Wata'ala)* 41-50 kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi<br>Darasa la tatu na radio | |
| 2.0 Kuthamini Qur'an na mafundisho yake | 2.1 Kumudu misingi ya kufahamu na kusoma Qur'an | (a) Kuhusianisha sauti na herufi yenye *Shadda* (ّ) ب→ b-b (**b**-imerudiwa mara mbili, mfano: رَبِّ = *rabbi* | **Kitanza ndimi:** Waongoze wanafunzi kusoma maneno/ silabi zenye herufi yenye sauti ya *shadda* | Kuhusianisha sauti na herufi yenye *Shadda* kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi<br>Darasa la Tatu | 15 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughul za Ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kuhusianisha sauti na herufi yenye **Maddah (/ ـا ـو / ـي )** ya kurefusha sauti) Maddah haikai juu ya **Ba (ب)** moja kwa moja, bali huja baada ya **Ba** ikiwa imewekewa haraka yake. **Baa (بَا) maddah** ya **Alif→ baa** (sauti ya **a** inarefushwa) **Buu (بُو) maddah** ya **Waw→buu** (sauti ya **u** inarefushwa)] Bii (بِي) – maddah ya Yaa → bii (sauti ya i inarefushwa) | **Kitanza ndimi:** Waongoze wanafunzi kusoma maneno/ silabi zenye herufi yenye sauti ya *madda* | Kuhusianisha sauti na herufi yenye **Maddah (ـا / ـو / ـي)** kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tatu | |
| | | (c) Kuhusianisha sauti na herufi yenye **Sukuun (ْ)** mfano: بْ → **b** tu bila sauti ya mwisho. Sauti inakatika ghafla— hakuna a, i, u. Mfano: اِذْهَبْ **(idh-hab)** | **Kitanza ndimi:** Waongoze wanafunzi kusoma maneno/ silabi zenye herufi yenye sauti ya *sukuni* | Kuhusianisha sauti na herufi yenye **Sukuun (ْ)** kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tatu | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughul za Ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2.2 Kusoma sura teule (*Nasr, Kafiruun na Kawthar* ) | (a) Kusoma na kutafsiri sura teule (*Nasr, Kafiruun na Kawthar* ) | **Midia:** Waongoze wanafunzi kusikiliza usomaji wa sura teule kifaa cha TEHAMA kisha waelekeze wasome mmoja mmoja huku ukiwasikiliza na kurekebisha kasoro zinazojitokeza. | Kusoma na kutafsiri sura teule (*Nasr, Kafiruun na Kawthar* ) kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa Tatu | 10 |
| | | (b) Kueleza ujumbe wa sura teule (*Nasr Kawthar*) | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kusoma matini juu ya tafsiri ya sura teule kisha kujadiliana kuhusu ujumbe unaopatikana katika sura hizo. | Kueleza ujumbe wa sura teule (*Nasr–Kawthar*) kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tatu | |
| 3.0 Kutekeleza ibada | 3.1 Kufafanua namna ya kutekeleza ibada ya swala | (a) Kuonesha namna ya kutayammamu kwa vitendo | **Onesho mbinu:** waoneshe wanafunzi picha zilizo katika mfuatano wa mtu anayetayamamu uwaongoze kutambua kila kitendo katika picha hizo.<br>**Igizo:** wongoze wanafunzi kuigiza kutayammamu hatua kwa hatua. | Kuonesha namna ya kutayammamu kwa vitendo kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tatu | 10 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughul za Ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kuonesha namna ya kuswali kwa vitendo (swala ya rakaa mbili, tatu na nne) | **Onesho mbinu:** waoneshe wanafunzi picha zilizo katika mfuatano wa mtu anayeswali uwaongoze kutambua kila kitendo katika picha hizo. **Igizo:** wongoze wanafunzi kuigiza kuswali hatua kwa hatua | Kuonesha namna ya kuswali kwa vitendo (swala ya rakaa mbili, tatu na nne) kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tatu | |
| | 3.2 Kuishi kwa Kumuiga Mtume (*Swallallaahu 'Alayhi Wasallam)* | (a) Kusoma dua za kila siku (dua ya kuingia msikitini, kutoka msikitini, kuanza kusoma) | **Onesho mbinu:** Waoneshe video ya usomaji kisha waongoze kusoma dua hizo. | Kusoma dua za kila siku (dua ya kuingia msikitini, kutoka msikitini, kuanza kusoma,) kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tatu | 8 |
| | | (b) Kuiga tabia njema ya Mtume (*Swallallaahu 'Alayhi Wasallam*) {kusaidia masikini, kuwaheshimu wakubwa n.k) | **Onesho mbinu:** Waongoze wanafunzi Kuiga tabia njema ya Mtume (*Swallallaahu 'Alayhi Wasallam*) { kusaidia masikini, kuwaheshimu wakubwa n.k) | Kuiga tabia njema ya Mtume (*Swallallaahu 'Alayhi Wasallam*) {kusaidia masikitini, kuwaheshimu wakubwa n.k) zimeigwa | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tatu | |
| 4.0 Kuthamini na kutumia Historia ya Uislamu | 4.1 Kufafanua mitume waliotajwa katika Qur'an | (a) Kutaja majina ya mitume waliotajwa katika Qur'an | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi kisha waulize maswali kuhusu majina ya mitume | Kutaja majina ya mitume waliotajwa katika Qur'an kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tatu | 9 |
| | | (b) Kueleza jinsi Adam (*Alayhis Salaam*) alivyoumbwa na kuletwa hapa ulimwenguni | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi kisha waulize maswali kuhusu jinsi Adam (Alayhis Salaam) alivyoumbwa na kuletwa hapa ulimwenguni | Kueleza jinsi Adam (*Alayhis Salaam*) alivyoumbwa na kuletwa hapa ulimwenguni kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tatu | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughul za Ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopende-kezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazope ndekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 4.2 Kufafanua namna Mtume *(Swallallaahu 'Alayhi Wasallam*) alivyofundisha Uislamu | (a) Kueleza hali ya kijamiii iliyokuwepo Makka kabla ya kuzaliwa Mtume (Swallallaahu 'Alayhi Wasallam) | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi wasome matini, kisha wabainishe na kujadili hali ya jamii ya Makka kabla ya kuzaliwa Mtume (*Swallallaahu 'Alayhi Wasallam*) | Kueleza hali ya kijamiii iliyokuwepo Makka kabla ya kuzaliwa Mtume (*Swallallaahu 'Alayhi Wasallam*) kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tatu | 10 |
| | | (b) Kueleza jinsi malezi ya mtume yalivyomuandaa kwa utume | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi wasome matini, kisha wabainishe na kujadili malezi ya Mtume na kuonesha kuwa yalikuwa ni maandalizi ya kupewa utume | Kueleza jinsi malezi ya mtume yalivyomuandaa kwa utume kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tatu | |

## Darasa la IV

**Jedwali Na.3:** *Maudhui ya Darasa la IV*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughul za Ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kuishi kwa kumpwekesha Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) | 1.1Kufafanua nguzo za imani | (a) Kusoma majina ya Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) 51-60 | **Onesho mbinu:** Tamka majina ya Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) 51-60 kwa sauti kwa kasi mwafaka kulingana na umri wa wanafunzi wako, (matamshi sahihi). Kisha waongoze wanafunzi kutamka | Kusoma majina ya Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) 51-60 kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Nne | 16 |
| | | (b) Kubainisha sifa na kazi za Malaika | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi kisha waulize maswali kuhusu sifa na kazi za Malaika | Kubainisha sifa na kazi za Malaika kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Nne | |
| | | (c) Kueleza faida za kuamini Malaika | **Majadiliano**: Waongoze wanafunzi kujadili faida za kuamini Malaika kwa kuzingatia kazi zao. | Kueleza faida za kuamini Malaika kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Nne | |
| | | (d) Kubainisha vitabu vya Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) vilivyotajwa katika Qur'an | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi, kisha wabainishe majina ya vitabu na mitume waliotere-mshiwa vitabu hivyo | Kubainisha vitabu vya Allah (*Subhaanahu Wata'ala*) vilivyotajwa katika Qur'an kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Nne | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughul za Ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2.0 Kuthamini Qur'an na kufuata mafundisho yake | 2.1 Kumudu misingi ya kufahamu na kusoma Qur'an | (a) Kubainisha adabu za usomaji Qur'an na kusoma kwa kuzizingatia | **Onesho mbinu:** kwa kuzingatia adabu za usomaji Qur'an waongoze wanafunzi kusoma sura fupi kwa kufuatisha. kisha waongoze wasome wenyewe mmoja mmoja. | Kubainisha adabu za usomaji Qur'an na kusoma kwa kuzingatia kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Nne | 8 |
| | | (b) Kubainisha majina ya Qur'an | **Majadiliano**: Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi kuhusu majina ya Qur'an kisha<br>**Igizo dhima:** Waongoze wanafunzi kuigiza majina ya Qur'an na kila mmoja kujigamba kwa kuzingatia maana ya jina husika. | Kueleza majina ya Qur'an kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Nne | |
| | 2.2 Kusoma sura teule (*Mau'un, Quraysh, Fiyl, Humazah na Asri*) | (a) Kusoma na kutafsiri sura teule (*Mau'un, Quraysh, Fiyl, Humazah na Asri*) | **Midia:** Waongoze wanafunzi kusikiliza usomaji wa sura teule kupitia kifaa cha TEHAMA kisha waelekeze mmoja mmoja asome huku ukiwasikiliza na kurekebisha kasoro zinazojitokeza | Kusoma na kutafsiri sura teule (*Mau'un, Quraysh, Fiyl, Humazah na Asri*) kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Nne | 16 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughul za Ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kueleza ujumbe wa sura teule (*Mau'un, Quraysh, Fiyl, Humazah na Asri*) | Majadiliano: Waongoze wanafunzi kusoma matini juu ya tafsiri ya sura teule kisha kujadiliana kuhusu ujumbe unaopatikana katika sura hizo. | Kueleza ujumbe wa sura teule (*Mau'un, Quraysh, Fiyl, Humazah na Asri*) kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Nne | |
| 3.0 Kutekeleza ibada | 3.1 Kufafanua namna ya kutekeleza ibada ya swala | (a) Kubainisha sifa za maji yanayofaa kujitoharishia | **Maswali na Majibu:** Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi kuhusu sifa za maji yanayofaa kutoharishia kisha kujibu maswali kuhusiana na matini waliyosoma<br>**Picha na Maelezo**: Chora picha za matenki mawili ya maji, moja lenye ujazo wa lita 200 na lingine lita 100. Katika matenki yote onesha mzoga wa panya. Waongoze wanafunzi kutambua sifa ya maji mengi na maji machache. | Kubainisha sifa za maji yanayofaa kujitoharishia kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Nne | 4 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughul za Ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopende-kezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazope ndekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b)Kutoharisha nguo yenye najisi | **Picha na Maelezo:** Chora picha ya watu wawili, mmoja anashikilia nguo huku mwenzake anamwagilia maji, kisha uwaongoze wanafunzi wachunguze picha hiyo, kisha uwaongoze waigize kutoharisha nguo wakiwa wawili wawili. | Kutoharisha nguo yenye najisi kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Nne | |
| | 3.2 Kuishi kwa kumuiga Mtume Muhammad *(Swallallaahu 'Alayhi Wasallam)* | (a) Kusoma dua za kila siku (chafya, mtu anapokasirika, kumshukuru mtu aliyekufanyia wema, dua wakati wa mafadhaiko) | **Onesho mbinu:** Waoneshe video ya usomaji kisha waongoze kusoma dua hizo. | Kusoma dua za kila siku (chafya, mtu anapokasirika, kumshukuru mtu aliyekufanyia wema, dua wakati wa mafadhaiko) kumefanyika. | Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Nne | 10 |
| | | (b) Kueleza adabu za kuingia chooni na kustanji | **Onesho mbinu:** Waoneshe wanafunzi namna ya kustanji na kuingia chooni kwa kuzingatia adabu za Kiislamu au picha uliyoiandaa, kisha waongoze waingie chooni kwa kuzingatia adabu za Kiislamu | Kueleza adabu za kuingia chooni na kustanji kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Nne | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughul za Ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopende-kezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazope ndekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 4.0 Kuthamini na kutumia Historia ya Uislamu | 4.1 Kufafanua Mitume waliotajwa katika Qur'an | a) Kubainisha kaumu zilizoanga-mizwa {Ad, Thamud, Lut na Madian} | **Changanyakete**: Gawa matini tofauti katika vikundi vinne (Ad, Thamud, Lut, Madian) Waongoze wanafunzi kusoma na kuandika waliyosoma katika matini hizo. Kisha kila kikundi kihakikishe kinasoma kazi zote na kueleza yaliyomo katika matini husika | Kubainisha kaumu zilizoanga-mizwa kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Nne | 10 |
| | | (b Kubainisha mafunzo kutokana na kaumu zilizoanga-mizwa | **Majadiliano**: Waongoze wanafunzi kujadiliana kwa kutumia matini walizosoma kuona madhara ya kukiuka amri za Allah *(Subhaanahu Wata'ala)* na kuwa Allah anao uwezo usio na mipaka. | Kubainisha mafunzo kutokana na kaumu zilizoanga-mizwa kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Nne | 4 |
| | 4.2 Kufafanua namna Mtume Muhammad *(Swallallaahu 'Alayhi Wasallam)* alivyofu-ndisha Uislamu | a) Kueleza jinsi Malezi ya Mtume Muhammad *(Swallallaahu 'Alayhi Wasallam)* yalivyomu-andaa kwa utume | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi, kisha waulize maswali kuhusu jinsi malezi ya Mtume Muhammad *(Swallallaahu 'Alayhi Wasallam)* yalivyomua-ndaa kwa utume | Kueleza jinsi Malezi ya Mtume Muhammad *(Swallallaahu 'Alayhi Wasallam)* yalivyomu-andaa kwa utume kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Nne | 6 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughul za Ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kueleza mafunzo yanayopatikana kutokana na jinsi Malezi ya Mtume Muhammad *(Swallallaahu 'Alayhi Wasallam)* *Swallallaahu 'Alayhi Wasallam)* yalivyomuandaa kwa utume | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi kuhusu jinsi Malezi ya Mtume Muhammad *(Swallallaahu 'Alayhi Wasallam)* yalivyomuandaa kwa utume | Kueleza jinsi Malezi ya Mtume Muhammad *(Swallallaahu 'Alayhi Wasallam)* yalivyomuandaa kwa utume kumefanyika | Kadi<br>Chati<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Nne | |
| | | (c) Kuonesha namna ya kuswali jamaa | **Picha na maelezo: Onesho mbinu:** Waelekeze wanafunzi wachunguze picha zilizo katika mfuatano wa watu wanaoswali jamaa, kisha **Igizo:** waongoze wanafunzi kuigiza kuswali jamaa (watu, 2, 3 na 4) | Kuonesha namna kuswali jamaa kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tano | |

**Darasa la V**

**Jedwali Na.4:** *Maudhui ya Darasa V*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughul za Ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kuishi kwa kumpwekesha Allah *(Subhaanahu Wata'ala)* | 1.1 Kufafanua nguzo za imani | (a) Kusoma majina ya Allah *(Subhaanahu Wata'ala)* 61-80) | **Onesho mbinu:** Tamka majina ya Allah *(Subhaanahu Wata'ala)* 61-80 kwa sauti kwa kasi mwafaka kulingana na umri wa wanafunzi wako, (matamshi sahihi). Kisha waongoze wanafunzi kutamka | Kusoma majina ya Allah *(Subhaanahu Wata'ala)* 61-80 kumefanyika | Chati Kadi Vifaa vya TEHAMA Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tano | 10 |
| | | (b) Kueleza sifa na kazi za Mitume | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi kisha waulize maswali kuhusu sifa na kazi za mitume | Kueleza sifa na kazi za Mitume kumefanyika | Chati Kadi Vifaa vya TEHAMA Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tano | |
| | 1.2 Kuchambua dhana ya shirki | (a) Kubainisha matendo ya kishirikina kama kutambika na kusujudia sanamu) | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi kisha waulize maswali kuhusu matendo ya kishirikina | Kubainisha matendo ya kishirikina kama kutambika na kusujudia sanamu kumefanyika | Chati Kadi Vifaa vya TEHAMA Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tano | 4 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughul za Ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kueleza namna ya kujikinga na ushirikina | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kujadiliana kwa kutumia matini namna ya kujikinga na ushirikina, kisha waulize maswali | Kueleza namna ya kujikinga na ushirikina kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tano | |
| 2.0 Kuthamini Qur'an na kutumia mafundisho yake | 2.1 Kumudu misingi ya kufahamu na kusoma Qur'an | (a) Kubainisha muundo wa Qur'ran (aya,sura, juzuu) | **Kazimradi:** Waongoze wanafunzi kwa kutumia msahafu kutambua aya, sura na Juzuu<br>**Maswali na majibu** Waongoze wanafunzi kueleza muundo wa sura na juzuu | Kubainisha muundo wa Qur'ran (aya, sura, juzuu) kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tano | 6 |
| | | (b) Kueleza sifa za Qur'an | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi kisha waulize maswali kuhusu sifa za Qur'an | Kueleza sifa za Qur'an kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tano | |
| | 2.2 Kusoma sura teule (Takathur -Bayyinah) | (a) Kusoma na kutafsiri sura teule (Takathur -Bayyinah) | **Midia**: Waongoze wanafunzi kusikiliza usomaji wa sura teule kwa kutumia kifaa cha TEHAMA kisha waelekeze wasome mmoja mmoja huku ukiwasikiliza na kurekebisha kasoro zinazojitokeza. | Kusoma na kutafsiri sura teule *(Takathur -Bayyinah)* kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tano | 16 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughul za Ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kueleza ujumbe wa sura teule *(Takathur -Bayyinah)* | Majadiliano: Waongoze wanafunzi kusoma matini juu ya tafsiri ya sura teule kisha kujadiliana kuhusu ujumbe wa sura hizo. | Kueleza ujumbe wa sura teule *(Takathur - Bayyinah)* kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tano | |
| 3.0 Kutekeleza ibada | 3.1 Kufafanua namna ya kutekeleza ibada ya swala | (a) Kubainisha masharti ya swala | **Ramani ya dhana:** Waongoze wanafunzi kupitia mchoro kubainisha masharti ya swala | Kubainisha masharti ya swala kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tano | 10 |
| | | (b) Kubainisha visomo na vitendo vya swala | **Ramani ya dhana:** Waongoze wanafunzi kupitia mchoro kubainisha matendo na visomo vya swala | Kubainisha visomo na vitendo vya swala kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tano | |
| | | c) Kuonesha namna ya kuswali na kuswalisha swala ya jamaa | **Picha na maelezo: Onesho mbinu:** Waelekeze wanafunzi wachunguze picha zilizo katika mfuatano wa watu wanaoswali jamaa, kisha **Igizo:** wongoze wanafunzi kuigiza kuswali jamaa (watu, 2, 3 na 4) | Kuonesha namna ya kuswali na kuswalisha swala ya jamaa kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tano | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughul za Ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 3.2 Kuishi kwa kumuiga Mtume Muhammad *(Swallallaahu 'Alayhi Wasallam)* | (a) Kusoma dua za kila siku (kuwaombea wazazi, dua za asubuhi na jioni, kuomba msamaha) | **Onesho mbinu:** Waoneshe video ya usomaji kisha waongoze kusoma dua hizo. | Kusoma dua za kila siku (kuwaombea wazazi,dua za asubuhi na jioni, kuomba msamaha) kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tano | 10 |
| | | (b) Kubainisha adabu za kula Kiislamu | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi kisha waulize maswali kuhusu adabu za kula Kiislamu Kisha waongoze waigize kula kwa kuzingatia adabu za Kiislamu | Kubainisha adabu za kula Kiislamu kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tano | |
| 4.0 Kuthamini na kutumia Historia ya Uislamu | 4.1 Kufafanua Mitume waliotajwa katika Qur'an | (a) Kueleza kisa cha Nabii Yunus *(Alayhis Salaam)* na mafunzo yanayopatikana | **Masimulizi:** Simulia kisa cha nabii Yunus *(Alayhis Salaam)* kisha **Majadiliano**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili mafunzo yanayopatikana kutokana na kisa walichosikiliza | (a) Kueleza kisa cha Nabii Yunus *(Alayhis Salaam)* na mafunzo yanayopatikana kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tano | 8 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughul za Ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopende-kezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazope ndekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kueleza kisa cha Nabii Yusuf (Alayhis Salaam) na mafunzo yanayo-patikana | **Masimulizi:** Simulia kisa cha nabii Yusuf (Alayhis Salaam) kisha **Majadiliano**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili mafunzo kutokana na kisa walicho-sikiliza | (b) Kueleza kisa cha Nabii Yusuf (Alayhis Salaam) na mafunzo yanayo-patikana kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tano | |
| | 4.2 Kufafanua jinsi Mtume Muhammad (Swallallaahu '*Alayhi Wasallam)* alivyo-fundisha Uislamu | a) Kueleza matukio ya kabla na wakati Mtume *(Swallallaahu 'Alayhi Wasallam)* anapokea wahyi wa kwanza | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi kisha waulize maswali kuhusu jinsi Mtume *(Swallallaahu 'Alayhi Wasallam)* alivyoanza kupokea wahyi | Kueleza matukio ya kabla na wakati Mtume *(Swallallaahu 'Alayhi Wasallam)* anapokea wahyi wa kwanza kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tano | 6 |
| | | (b) Kueleza mafunzo yanayo-patikana kutokana na Mtume *(Swallallaahu 'Alayhi Wasallam)* alivyoanza kupokea wahyi | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi kisha waulize maswali kuhusu mafunzo yanayo-patikana kutokana na jinsi Mtume *(Swallallaahu 'Alayhi Wasallam)* alivyoanza kupokea wahyi | Kueleza mafunzo yanayo-patikana kutokana na Mtume *(Swallallaahu 'Alayhi Wasallam)* alivyoanza kupokea wahyi kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tano | |

## Darasa la VI

**Jedwali Na.5:** *Maudhui ya Darasa VI*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughul za Ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kuishi kwa kumpwekesha Allah *(Subhaanahu Wata'ala)* | 1.1 Kufafanua nguzo za imani | (a) Majina ya Allah *(Subhaanahu Wata'ala)* 81-99 | **Onesho mbinu:** Tamka majina ya Allah *(Subhaanahu Wata'ala)* 81-99 kwa sauti kwa kasi mwafaka kulingana na umri wa wanafunzi wako, (matamshi sahihi). Kisha waongoze wanafunzi kutamka | Kusoma majina ya Allah *(Subhaanahu Wata'ala)* 81-99 kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Sita | 16 |
| | | (b) Kubainisha alama za siku ya kiyama | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi kisha waulize maswali kuhusu alama za kutokea siku ya kiyama | Kubainisha alama za kutokea siku ya kiyama kumefanyika | | |
| | | (c) Kueleza matukio makubwa ya siku ya kiama | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi kisha waulize maswali kuhusu matukio makubwa ya siku ya kiama | Kueleza matukio makubwa ya siku ya kiama kumefanyika | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughul za Ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopende-kezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazope ndekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (d) Kubainisha faida za kuamini siku ya kiama | **Majadiliano**: Waongoze wanafunzi kujadiliana kwa kutumia matini faida za kuamini siku ya kiama | Kubainisha faida za kuamini siku ya kiama kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Sita | |
| | | (e) Kueleza maana ya kuamini Qadar na faida zake | **Maswali na majibu**: Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi kisha waulize maswali kuhusu maana ya kuamini Qadar na faida zake | Kueleza maana ya kuamini Qadar na faida zake kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Sita | |
| 2.0 Kuthamini Qur'an na kutumia mafundisho yake | 2.1 Kumudu misingi ya kufahamu na kusoma Qur'an | (a) Kubainisha misingi ya kuifahamu Qur'an | **Majadiliano**: Waongoze wanafunzi kujadiliana kwa kutumia matini misingi ya kuifahamu Qur'an, kisha waulize maswali | Kubainisha misingi ya kuifahamu Qur'an kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Sita | 4 |
| | | (b) Kueleza umuhimu wa Qur'an katika maisha ya Muislamu | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi kisha waulize maswali kuhusu umuhimu wa Qur'an katika maisha ya Muislamu | Kueleza umuhimu wa Qur'an katika maisha ya Muislamu kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Sita | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughul za Ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopende-kezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazope ndekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2.2 Kusoma sura teule *(Qadr -Dhuhaa)* | a) Kusoma na kutafsiri sura teule *(Qadr-Dhuhaa)* | **Midia:** Waongoze wanafunzi kusikiliza usomaji wa sura teule kwa kutumia kifaa cha TEHAMA kisha waelekeze wasome mmoja mmoja huku ukiwaikiliza na kurekebisha kasoro zinazo-jitokeza | Kusoma na kutafsiri sura teule *(Qadr-Dhuhaa)* kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Sita | 20 |
| | | (b) Kueleza ujumbe wa sura teule *(Qadr -Dhuhaa)* | **Majadiliano**: Waongoze wanafunzi kusoma matini juu ya tafsiri ya sura teule kisha kujadiliana juu ya ujumbe wa sura hizo | Kueleza ujumbe wa sura teule (Qadr Dhuhaa) kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Sita | |
| 3.0 Kutekeleza ibada | 3.1 Kutekeleza ibada ya funga | (a) Kubainisha mwanzo na mwisho wa Funga ya mwezi wa Ramadhani | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi kisha waulize maswali kuhusu mwanzo na mwisho wa mwezi wa Ramadhani | Kubainisha mwanzo na mwisho wa Funga ya mwezi wa Ramadhani kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Sita | 4 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughul za Ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kubainisha nguzo za funga | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi kisha waulize maswali kuhusu nguzo za funga | Kubainisha nguzo za funga kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Sita | |
| | | (c) Kubainisha mambo ya Sunnah katika mwezi wa Ramadhani | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi kisha waulize maswali kuhusu mambo ya sunnah katika mwezi wa Ramadhani | Kubainisha mambo ya Sunnah katika mwezi wa Ramadhani kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Sita | |
| | 3.2 Kuishi kwa kumuiga Mtume Muhammad *(Swallallaahu 'Alayhi Wasallam)* | (a) Kusoma dua za kila siku (kutoka nyumbani, kurudi nyumbani, kuomba afya, kuomba msamaha n.k) | **Onesho mbinu:** Waoneshe video ya usomaji kisha waongoze kusoma dua hizo. | Kusoma dua za kila siku (kutoka nyumbani, kurudi nyumbani, kuomba afya kuomba msamaha) kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Sita | 10 |
| | | (b) Kueleza madhara ya tabia mbaya (kujenga chuki, kukosa baraka za Allah *(Subhaanahu Wata'ala),* kukosa msaada n.k) | **Majadiliano**: Waongoze wanafunzi kujadiliana kwa kutumia matini kuhusu madhara ya tabia mbaya (kujenga chuki, kukosa baraka za Allah *(Subhaanahu Wata'ala),* kukosa msaada n.k) | Kueleza madhara ya tabia mbaya (kujenga chuki, kukosa baraka za Allah *(Subhaanahu Wata'ala)* kukosa msaada n.k) kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Sita | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughul za Ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopende-kezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazope ndekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 4.0 Kuthamini na kutumia Historia ya Uislamu | 4.1 Kutambua Mitume waliotajwa katika Qur'an | (a) Kueleza kisa cha Nabii Daud *(Alayhis Salaam)* mafunzo yanayopa-tikana | **Masimulizi:** Simulia kisa cha Nabii Yunus *(Alayhis Salaam)* kisha waulize maswali kuhusu masuala muhimu katika kisa hicho | Kueleza kisa cha Nabii Daud *(Alayhis Salaam)* mafunzo yanayopa-tikana kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Sita | 8 |
| | | (b) Kueleza kisa cha Nabii Sulaiman *(Alayhis Salaam)* na mafunzo yanayopa-tikana | Kueleza kisa cha Nabii Sulaiman *(Alayhis Salaam)* na mafunzo yanayopa-tikana | Kueleza kisa cha Nabii Sulaiman *(Alayhis Salaam) na* mafunzo yanayopa-tikana kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Sita | |
| | 4.2 Kufafanua namna Mtume *(Swallallaahu 'Alayhi Wasallam)* alivyofundisha Uislamu | (a) Kueleza jinsi Mtume *(Swallallaahu 'Alayhi Wasallam)* alivyoanza kufikisha ujumbe wa Uislamu kwa watu | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kujadiliana kwa kutumia matini jinsi Mtume *(Swallallaahu 'Alayhi Wasallam)* alivyoanza kufikisha ujumbe wa Uislamu kwa watu, kisha waulize maswali | Kueleza jinsi Mtume *(Swallallaahu 'Alayhi Wasallam)* alivyoanza kufikisha ujumbe wa Uislamu kwa watu kumefanyika | Chati<br>Kadi<br>Vifaa vya TEHAMA<br>Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Sita | 8 |

## Bibliografia


Islamic Education Panel. (2012). *Muhtasari wa elimu ya dini ya Kiislamu: Elimu ya msingi darasa la 1–VII*.

Mauritius Institute of Education. (2015). *National curriculum framework grades 1–6*.

Sheikh Abdullah Saleh Farsy. (1987). *Qur'an tukufu: Tafsiri na maana yake kwa lugha ya Kiswahili*.

Taasisi ya Elimu Tanzania. (2023). *Mtaala wa elimu ya msingi darasa la III–VI*.